

# UKIUKAJI WA HAKI ZA BINADAMU HAUKUBALIWI KWENYE

Kikundi chetu kinakuza usawa na heshima miongoni mwa wanachama kwa sababu hii inawawezesha kuboresha maisha yao na kulinda mazingira wanamoishi na kufanya kazi.

Ikiwa kikundi, au vitendo, sheria na sera zake zimemdhuru mtu yeyote, tunataka kushughulikia masuala haya na kuwasaidia wale walioathirika.

**Ifichue, isuluhishe na ikomeshe!** ✓



## MASUALA YA HAKI ZA BINADAMU NI:

Tabia inayodhuru mtu yeyote, mahali popote, ambayo inatokana na shughuli, sheria au sera za shamba.

**Ifichue, isuluhishe na ikomeshe!** ✓



*Kuwatumikisha watoto*

*Kazi ya kulazimishwa*

*Ubaguzi*

*Vurugu na unyanyasaji kazini*

Kuwatumikisha watoto, kazi za kulazimishwa, ubaguzi, na vurugu na unyanyasaji kazini hudhuru watu na kikundi.

**Ifichue, isuluhishe na ikomeshe!** ✓

## UNAPASWA KUWASILIANA NA NANI?

Kamati ya Malalamiko na kamati ya Kutathmini-na-Kushughulikia, wakiwemo wanachama wa kikundi, huchunguza visa vilivyoriipotiwa ili kujaribu kurekebisha madhara yoyote ambayo yamefanyika na kutoa msaada.

### Wajumbe wa Kamati yako:

- Watajibu ndani ya siku 2
- Wataweka ripoti yako ya kisa kwa siri
- Watakulinda dhidi ya ulipizaji kisasi
- Watashughulikia malalamiko bila kufichua utambulisho

### Wajumbe wa kamati yako ni:

Kamati ya Malalamiko : .....

Kamati ya Kutathmini-na-Kushughulikia : .....

Wasiliana na (Piga Simu/SMS): .....

**Ifichue, isuluhishe na ikomeshe!**

## MASUALA MENGI YANAWENZA KURIPOTIWA

Tabia ya kudhuru mtu yeyote, popote pale, inayotokana na shughuli, sheria au sera za kikundi.

Nina wasiwasi kuhusu mfanyakazi mchanga aliyeajiriwa kwa kazi ya mavuno kwenye mashamba ya kikundi. Nadhani anapigwa.

Inspekta alipotutembelea, alitupigia kelele na kutukemea. Nilihisi hofu.

Mafunzo yanaandaliwa mbali sana nasi, lakini wasimamizi hawafanyi mipango ya kuandaa mafunzo yoyote katika eneo letu.

Kwa nini wakufunzi wote wa kikundi wanatoka kijiji kimoja? Hakuna mtu mwingine aliyepewa nafasi hiyo.



*Maji machafu kutoka shambani bado yanachafua mto ingawa tumejulisha shamba kuhusu hilo.*

Hawa ni wasichana wadogo wakibeba mizigo mizito sana ya maji kurudi nyumbani na wavulana wakitumia mapanga kukata kuni. Hii ni hatari kwao!

Nilishuhudia vikundi vya watoto wakifanya kazi siku nzima katika baadhi ya mashamba wakati wa msimu wa mavuno. Hawakuzungumza lugha yetu ya kienyeji, wanatoka nchi tofauti.


Wanawake wanashauriwa kutoomba majukumu ya usimamizi na wasimamizi wa sasa katika kikundi.

Nimeshuhudia watoto wenye umri wa miaka 8 wakifanya kazi kwenye shamba la familia zao wakati wa saa za shule.

## JE, NINI KINGINE UNAWENZA KUFANYA?

Ikiwa kikundi – matendo, sheria na sera zetu – zinadhuru mtu yeyote, tunataka kurekebisha masuala haya na kuwasaidia wale walioathirika.

Wanachama wa K&K na Kamati za Malalamiko wanashirikiana ili kuzuia madhara.



- Unaweza kusaidia kwa:**
- Kuwachagua na kuwasaidia wajumbe wa kamati yako
  - Kujiunga na kamati.



**Ifichue, isuluhishe na ikomeshe!**